# NISHANI YA PAKA

**YALIYOMO**


1. MAHITAJI – (MAPYA NA YA ZAMANI)
2. UTANGULIZI
    - PAKA KATIKA BIBLIA
    - TABIA ZA PAKA
    - PAKA WA PORINI
    - PAKA WA PORINI WA AFRIKA KUSINI
        - CHUI
        - CHITA
        - SIMBA
        - LYNX – PAKA MWITU
        - SERVAL – NGAWA
        - PAKA WA PORINI WA AFRIKA
        - PAKA MWEUSI MIGUU MIEUSI
        - LIGER NA TIGLON

    WANYAMA WA AFRIKA KUSINI AMBAO WANAFANANA NA PAKA LAKINI SI PAKA

    - CHUI MKUBWA
    - PANTHER MWEUSI
    - COUGAR
    - CHUI WA AMERIKA YA KUSINI (JAGUAR)
    - PAKA WA BOB WA AMERIKA
    - PAKA
3.






**MAHITAJI**

Haya ndiyo mahitaji mapya kama yaliyoletwa kwa Nishani za Watafuta Njia, zilizotolewa na G.C mwaka 1990.
Mahitaji ya zamani yataendelea kutoka moja baada ya nyingine.

**MAHITAJI MAPYA**

1. Majina ya kabila la paka ni?
2. Ni kwa namna gain umbo la nyayo za mnyama mwenye kucha vinafanana na paka wote?
3. Kwa namna gani macho ya paka wote yanafanana?
4. Ndevu na mashavuni ya paka yana kazi gani?
5. Kwa namna gani masikio ya paka yanalindwa?
6. Taja aina nne za paka wanaofugwa, eleza kila mmoja
7. Paka wa kufugwa wanafaida gani kwa mwanadamu?
8. Taja aina saba ya paka wasiyofugwa. Watambue kila mmoja , elezea wanapatikana eneo gani la ulimwengu?
9. Ni mnyama gani anayejulikana kama mfalme wa wanyama? Taja aina nyingine ya paka wakubwa wa ulimwengu huu.

10. Elezea kisa cha **Androcles** na simba
11. Linganisha visa vinne katika Biblia mahali ambapo kundi la jamii ya paka linatajwa.

# MAHITAJI YA ZAMANI

1. Nini maana ya jina **Felidae**?
2. Taja tabia tatu za jamii ya paka
3. Ni jamii ipi ya paka inajulikana kama mfalme wa wanyama
4. Ni paka yupi ni mkubwa zaidi katika bara la Amerika?
5. Ni paka yupi anafahamika kuwa mkubwa duniani?
6. Ni aina ipi ya kundi la paka anayekimbia kwa kasi ya km 70 kwa saa
7. **Ecelot** anapatikana wapi?
8. Ni yupi anayeitwa kondoo mweusi wa jamii ya paka
9. Majina yapi matatu yaliyopewa paka wa Afrika wenye vishungi kwenye masikio
10. Tiger anapatikana wapi?
11. Jamii gani ya paka inapatikana Afrika kusini na ni adui wa panya wa miwa
12. Elezea mwonekano wa paka pori wa Afrika
13. Ni jamii ipi ya paka wa Afrika iliyepewa jina kwa sababu ya rangi ya miguu yake
14. Taja jina la mtumwa wa kirumi aliyeokolewa kwa kuwa rafiki wa simba
15. Taja visa vitatu vinavyopatikana katika Biblia ambavyo vinataja makundi ya jamii ya paka
16. Taja wanyama kumi walio jamii ya paka
17. Chakula kikuu cha paka ni nini?
18. Taja makundi mawili ya paka wa kufugwa
19. Ni paka yupi ni mzuri zaidi mwenye manyoya mafupi
20. Ni paka yupi ni mgeni kabisa katika paka wote wa kufugwa. Aina inayopatikana kwa nadra Mexico
21. Ni paka yupi aliyemjeuri, wakati mwingine anaitwa paka – panya
22. Paka wakufugwa wanafaida gani kwa mwanadamu?
23. Taja aina saba ya paka wa kufugwa
24. Elezea kisa juu ya paka

# UTANGULIZI

Swala la kujifunza paka ni la kuvutia sana, wanajulikana kama (jamii ya paka) **felines,** kabila ya paka jina la kisayansi "**felidae"**

Tunapata maelezo kuwa paka wametajwa katika historia ya misri mwanzoni mwa karne ya 13 BC. Hivyo haishangazi kusikia kuwa walitendewa kama viumbe vitakatifu, wachina nao walikuwa na paka mwanzo wa mwaka.yao

Siku za zamani paka waliwekwa katika meli ili kufukuza panya na mapanya book. Hivyo ilikuwa rahisi paka kusafirishwa toka nchi moja kwenda nyingine.

**PAKA KATIKA BIBLIA**

Nyakati za Biblia jamii ya paka inatajwa ni hatari lakini ni kweli pia visa vya ukuaji wa manyoya yao unaoongelewa na mafundisho mengi tunaweza kujifunza toka kwa paka. Yeremia 13:23

Swali linaulizwa je chui aweza kubadili madoa doa yake? Kama ilivyo kwa mwanadamu mwenye dhambi hawezi kujibadili isipokuwa kwa njia tu ya neema ya Yesu Kristo Daniel 7:6
Hosea 13:7
Mafungu hayo pia yanataja chui, yatafute katika Biblia yako yasome wewe mwenyewe. Mojawapo ya visa vya kusisimua ni wakati mtu anapokutana na simba. Tafakari juu ya Samsoni aliye ua simba kwa mikono Warumi 14:4 – 20. Daniel naye alitupwa katika tundu la simba lakini hawakumdhuru Daniel sura 6. kabla Daudi hajawa mfalme alimuua simba ambaye alikuwa anataka kushambulia kundi la kondoo za baba yake. 1Samwel 17: 34 – 37.

**TABIA YA PAKA**



Kwa namna gani tutaelewa kuwa paka ni paka? Yapo mambo ya kuweka maanani

1. Paka ni aina ya wanyama wa0itwa mamalia; wanapatikana nchi kavu peke yake; wengi wao katika hali yao ya kuishi porini wanaweza kuogelea inapowalazimu, na wengine wanapenda maji.
   - Paka wa kufuga, kwa namna nyingine hawataki maji
   - Paka kama sheria wanapenda kukwea miti lakini ni wa namna yake. Hii ni kw awale wa porini na wale wa kufugwa.

   Paka wanapenda kunoa kucha zao kwa kuzirudisha ndani ya kifuniko chake kwa kutaka kwao hasa wanapotembea. Wanazitoa nje wanapotaka kutenda kitu.



- Upenda kuzinoa kwenye matawi ya miti na wale wa kufugwa kwenye viti vya ndani/makochi.

Wana kucha tano miguu ya mbele na nne miguu ya nyuma.

- Kama sheria paka anatembea kwa utulivu bila kelele kulingana na ulaini/uololo wa kinga au aina ya sponji iliyo chini ya wayo wake.
- Mara nyingi wananyemelea mawindo yao na kurukia ama sivyo watawakimbia. Mara wanapofukuza hakuna kitakacho wasimamisha kwa lengo lao, angalia paka wako anavyonyatia ndege kwenye bustani. Paka anachukia mbwa.
- Mara nyingi paka wanavuta mawindo yao kwenda wanakolala, karibu na pango au juu ya mti.

Hawasumbuliwi na kitu kingine wanapokula chakula chao hawataki kushirikisha wengine chakula chao **isipokuwa familia yake tu**. Kilichobaki kinaachwa kwa mlo utakaofuata.



Paka mara nyingi wanatembea usiku. Hii inamaana kuwa wanajificha au kulala ndani ya vivuli vya miti wakati wa mchana na wanatoka nje wakati jua linapozama kwa mawindo. Paka wa kufugwa wanalala mahali penye joto au kwenye jua ili hali yake ya kuzunguka kuwinda ifanikiwe wakati wa usiku.

Paka wana macho yenye mwanga unaomulika kwenye mboni zao. Wanaona vizuri wakati wa usiku kwa sababu macho yao ni ya mviringo na makubwa yanayoruhusu nuru nyingi kuingia. Lakini hawaoni kabisa katika giza zito. Wakati wa mwanga wa jua macho yao yanapungua ili kuweka mwanya mdogo wa kutoa mwanga.



Kitu cha kuvutia juu ya macho ya paka ni kuwa zile kuta zilizoko nyuma zimezungushiwa na kitu kinachoitwa “**Guanin**” (kama mari ya ndege/chokaa) ambayo yana aina ya mngaro wa madini ya fedha au dhahabu. Mwanga unapopiga juu ya “guanine” hii chembe chembe hizo zinakuza na kutoa nuru na picha ambayo ilikuwa haionekani vizuri ina mlika kwenye kioo cha mboni au retina ndani ya jicho, ili kumwezesha kuona vizuri.

- Kuona, kusikia na kunusa vyote vina kuzwa vizuri wakati kuonja au radha yake ni dhaifu. Vyote hivi vinasaidia mchakato wa kutafuta chakula au mawindo yake.



Ndani ya masikio yake yapo manyoya ambayo yanadaka mara moja aina yoyote ya mtikisiko unaotoka hewani na kuelezea mnyama mwenendo hata ambao hawajawahi uona. Hii ni kama tendo la kujilinda kwa paka.

Jamii yote ya paka ina rangi aina ya milia, madoa madoa na kupambwa kwa namna yake. Wengine wanamadoa doa, wengine sawia, japo wawe na aina gani ya rangi inawasaidia kughiribu na kujificha kabisa kwa mazingira yao ili kwamba wasipokuwa wanatembea wasitambuliwe. Wanapowinda pia hawaonekani kama mwanga wa ghafla.

Paka ana meno 30 badala ya 40 kama alivyoumbwa, kwa namna nyingine wana mfupa mfupi wa taya huu ni wa lazima. Hayo meno ndiyo yaliyo imara na makali na ndiyo siraha zake za hatari sana pamoja na makucha yake makali hasa paka wa porini.

Wanayo manyoya marefu upande wa uso wake yanayojulikana kama “sharafa” au wayo wa tano wa paka. Unamsaidia mnyama kuhisi vitu Fulani gizani na kutoa mlio wa onyo. Bila vitu hivi hawezi kunyatia wanapokuwa katika mawindo, pia sharafa hizi zinatumika kama wakala wa vipimo. Kama sharafu hizi zinaweza kupita sehemu Fulani mwili wote utapitia hapo.

Paka kwa hali halisi ni wasafi, siku zote wanajilamba wenyewe na kujiosha. Angalia mama yao anavyo walamba watoto, anawasafisha, ana kitu kinachofanana na ubao wa kukwaruza katika ulimi wake ndiyo unaofanya program zote za kuosha na kusafisha.



Mkia wa paka kwa kawaida ni mrefu na uliyopinda wakati mwingine unapambwa na wingi wa manyoya. Unaonyesha tabia au hali ya paka aliyo nayo.

Anapoupindisha na kuuzungusha kwa nguvu na kuwa mgumu na ukanyooka anapokuwa ametishwa. Anapokuwa amefurahi unakuwa laini na unazunguka juu na chini. Pia mkia unampa uwiano mzuri anapokimbia, paka anayo hisia au tabia nyingi wanaweza kuunguruma kutoa mlio kama wa kulalamika wakatili wakati mwingine wanahamu ya kujua kila kitu kinacho wazunguka. Wanaonyesha mapenzi mema kwa wenzake na wanadamu, wanaitikia kwa urafiki na wanaweza kuwa mwenzi wa karibu mtii na rafiki. Wanaonyesha furaha yao, kujisikia kwao na furaha kwa kukoroma na kukanda chini nyayo zao, wengine ni mbwa walinzi kuliko mbwa wenyewe.

Wanapohisi hatari manyoya yao husimama, yanasisimka kabisa kama watakavyotumia makucha yao kuparura. Ingawa ni watiifu kwa asili hasa wale wa kufugwa, watapigana na adui wanapohusishwa. Anapokuwa ameshika kitu atafanya kelele ya kuunguruma, simba ndiye wanapiga kelele sana. Hasa wanapokuwa wanalea hii inaweza kuwa usumbufu na kuchafua hasa vichanga vinapokuwa nje wakati wa usiku.



Vitoto vinazaliwa vikiwa havioni na visivyo na lolote, ikifuatiwa kipindi kirefu cha kufundishwa na kujifunza, wanafundishwa toka mwanzo kuwa tayari na waangalifu na mazingira yao kama ipo hatari yoyote.

Wakubwa na watoto wanacheza pamoja watanguruma, wataparura lakini siyo kwa kuumizana watarukia juu ya migongo ya wakubwa, wataruka huku na huku, juu ya wenzao nk. Pia wanaweza kutesa wasiyo na hatia katika mchakato wa kuumiza.

Katika yote paka wanapenda kuwa peke yao, isipokuwa simba wanaozunguka kwa majivuno. Wale paka wa kufugwa watashikamana na mmoja tu, bwana wake na kufuatisha pia mazingira mapya na bwana mpya mwenye ugumu furani.

Paka wa porini ni wajanja, wakali na wawindaji hodari. Hawana mfupa wa shingoni katika maumbile ya paka atatua kwa miguu yake siku zote anapotupwa mahali au kuanguka akiwa na uwezo wa kucheza na kugeuza akili yake hewani akitua bila msukumo wowote.

**ANGALIA BAADHI YA PAKA WA PORINI WA DUNIA**

**PAKA WA PORINI – WILD CAT**

Afrika ya kusini tunayo aina saba ya paka wa porini

1. Simba
2. Chui duma – cheetah
3. Chui
4. Lynxes – paka mwitu mwenye macho makali
5. Paka wa porini wa Afrika
6. Serval – Ngawa
7. Paka mwenye miguu mieusi – Black footed cat.

**CHUI**

Chui anayejulikana kama (panther) chui mweusi wa Amerika, huyu ni paka wa usiku anayeonekana mara chache sana, anasifiwa sana Afrika na As**ia. Anataka kufanana na chui mdogo mwenye madoa ya milia (**tiger).

Ni mjanja sana na mwindaji katili lakini ni mnyama anayejificha kwenye mapango ya mawe na misitu minene ili asionekane kwa urahisi. Ni mpindaji miti hodari sana na siku zote hata mawindo yake anayapandisha juu ya matawi ya miti.



Amejenga vizuri sana siku zote anaonekana mwenye nguvu, kwa pigo moja anauwa wanayama wadogo. Katika paka wenye rangi ya milia yeye ndiye mkubwa zaidi, akiwa na ngozi ya njano ni wazi anapofanya kuparuza kwenye mwili huu wa kkuparuza wa rangi hiyo.



Koromeo lake ni jeupe, si kwamba ni vigumu kuliona lakini hata wakati anapobweka huwezi pia kusikia.



Masikio yake ni madogo juu ya kichwa yakiwa na sharafu ndefu kuna hali ya kuogofya katika kutazama kwake, hali ya kutisha sana

Ni mwepesi sana katika ardhi mara nyingi anakua juu ya miti na kusubiri mawindo yake yanapopita chini yake kwa namna ya pekee huruka bila kuogopa chochote. Mnyama huyu ni hatari na ana hali ya ukatili sana.

Atashambulia wanyama wakubwa zaidi ya  yeye ili kupata chakula. Ana waangalia wale wadogo na wadhaifu katika kundi atakao na kuwakamata. Anapenda sana nyani na mbweha., katika mazingira ambayo anakosa vyakula vya asili atakamata mbuzi na ng'ombe, ndiyo sababu hajulikani sana kwa wafugaji.

Majike yanakuwa ndiyo watafutaji wa chakula kwa madume, kama hatapata mawindo kwa watoto wake, majike mengi yatauwawa siyo kwa chakula bali tu kutaka kuona mizoga.

Chui kwa hali halisi ni wapweke, wataonekana tu na mwenzake wakati wa kujamiiana. Wanalazimika kuwa karibu na maji ingawa wanapendelea maeneo ya vichaka mahali wanapojificha na wakati mwingine juu ya miti.

**DUMA – (CHEETAHS)**



Makao yao makuu ni Afrika ya kusini bali pia kwa ajili ya biashara leo wamesafirishwa nchi nyingi. Wapo wanaotaka kubisha kuwa hawa ni daraja lao tu bali kwa ajili ya mazoezi, duma ni paka halisi. Ukweli ni kuwa yeye hawezi kurudisha ndani makucha yake kama walivyo wengine lakini hili halifanyi tumwondoe katika kundi la paka. Yeye hapendi miti.



Huyu paka anataka kufanana kama chui, lakini ana miguu mirefu, mwonekano wake ni wa usafi na ndiye mnyama anayekimbia kwa kasi sana kuliko wanyama wote. Anauwezo wa kukimbia maili 70 kwa saa au km 85 kwa saa kwa umbali mfupi. Hawezi kuendelea kwa muda mrefu.

Atafukuzia mawindo yake na kuyashika kabla hajachoka. Wanawinda wakiwa katika jozi nyakati za asubuhi kukingali na ubaridi, watauma mawindo yao shingoni ili watoe damu kwa haraka na kuanza kuburura kwenda kwenye makao ya wenzao.



Ni mnyama mjanja lakini muungwana siyo katili sana kama chui. Kuna tabia ya machozi chini ya macho yake inayompa mguso  kuwa kama analia. Mkia wake upo nyuma ukiwa umenyooka na kupinda kidogo anapokuwa anafukuza.

**SIMBA**

"LEO" au "LION" – Simba maana yake ni "mfalme" au utii, simba anajulikana kama mfalme wa wanyama, mnyama alaye nyama sana katika Afrika au Afrika kusini, kwa bahati mbaya tabia yake zaidi ni ya kujionyesha kuwa ni ya kifalme au ya kiutawala. Lakini kwa hali halisi ni mkorofi. Jike ndilo linawinda zaidi na dume linajiunga tu kusherekea.



Katika paka wote simba anadai utii kwa ajili ya umbo lake na mwonekano wake wa kifalme. Huyu kwa hakika ni mnyama wa Afrika amechukuliwa na kufugwa mahali pengi na hata katika mbuga zingine.

Simba anapigania ukubwa katika kundi kuna simba dume linalotawala na majike kadhaa na vichanga katika kiburi kidogo.

Simba hulala dhidi ya upepo wakati mawindo yake yanapokuwa karibu anaweza kupata harufu ya punda milia, swala, pongo lakini hasikii harufu ya simba mwenzake.

Majike kadhaa yanaweza kwenda maeneo tofauti na kutembea pole pole. Madume yanaweza kuja kutawanya mawindo na kuacha jike moja kukimbia. Hata twiga pia wanaweza kuwa mawindo ya simba bali si mara zote kwa sababu wanaogopa mateke ya twiga. Simba anapokuwa ameua, anategemea simba wenzake waje washirikiane chakula. Anaanza kula kwanza na baadaye majike na vitoto vinakuja kula kile kilichobakizwa.



Simba jike ana umbo dogo kuliko dume hana manyoya mengi ya shingoni kama dume. Hulala kimya na kusubiri na kumrukia bila kutoa tahadhari kwa nguvu anaparua kwa makucha yake anapomwona mnyama au binadamu asiye na shirika naye  aweza kutetemeka na kuzama kabisa.

Simba anapokula anaunguruma akionyesha kufurahia au kutoshelezwa. Simba hajisafishi kama ilivyo kwa paka wengine. Watakaa siku nzima baada ya kupata mawindo mazuri kabla hawajafanya mawindo mengine.

**LYNX – paka mwitu mwenye macho makali**

Huyu ni paka wenye majina mengi, mojawapo "paka mwekundu" kwa ajili ya ngozi yake yenye wekundu na uzuri wake. Pia anajulikana paka "mwenye kishungi" (Tafted – roolkat) Afrika. Mwenye masikio ya vishada au vishungi, kutokana na vishungi vilivyo katika masikio yake.



Huyu ni mnyama mwenye vishungi vilefu kuliko manyoya yake meusi kwenye masikio yaliyosimama, wakati wa kipupwe yeye anaonekana kama kahawia.
Paka huyu ana uso mrefu na mkia mnene usiyo mrefu sana aliye na miguu mirefu iliyojificha. Sauti yake inataka kufanana na paka wa kufugwa. Ni paka wa hatari sana, mwenye nguvu, mjanja na mwelevu na mkali kwa asili yake, mlafi kama chui, ni wakuogopwa wakati wote. Anasifika kwa hasira zake, hasa anapokuwa amepata mawindo au amechokozwa.

Atafanya lolote ili apate chakula hata kama ni kufukuza kuku au kanga na zizi la kondoo. Ana chukiwa na wakulima na kuna gharama katika kumtoka au kumuua.



Lynx, huyu anapendelea kuishi kwenye miamba ya milimani ili aweze kujilinda. Anawasiwasi na mwanadamu ingawa ni rahisi kushikika. Anapokuwa pangoni hawezi kutoka nje, kama mtoto mkorofi atarusha kelele na ngurumo na kuparura parura na kutema mate. Unapomwinda unapaswa kuwa mwangalifu kumsogelea anapokuwa katika hali hiyo.

**NGAWA – SERVAL (Tier boskat)**

Ni mwembamba lakini mnyama mzuri, anatishiwa uhai siku hizi, mpandaji mzuri wa miti na mawe, anapendelea kuwa kwenye ardhi anapokuwa anawinda wanyama wadogo nyakati za usiku.



- Ni mrukaji mzuri sana kwenye ardhi kutokana na uzito wake mdogo unaompatia faida.
- Miguu yake na mkia ni mfupi hii inamsaidia miondoko yake.
- Ana aibu lakini vitoto vyake vinaweza kuwa vya kufugwa na kuwa kama wanyama wa kufugwa.
- Ngozi yao ni aina ya njano inafanya kuwa na maumbo yasiyo ya kawaida na kuwa kwenye maumbo tofauti.

**PAKA WA PORINI WA AFRIKA**



Wanajulikana kama paka **kaffir,** siku zilizopita kulingana na jina la kisayansi (**felis caffra**). Huyu paka kwa Afrika anaitwa paka pori, Afrika ya kusini anajulikana kama “**vaalboskat**”

Asili yake ni Afrika wanapatikana karibu kila mahali toka Kasikazini hadi chini ya Jangwa la sahara.

Paka huyu ni mkali mwenye malengo. Unapaswa utahadhari kuwa katika njia yake kweli ni wa porini, ana hasira kali na mbaya atakwaruza chini akiwa na maana. Anajificha katika vichaka vizito na kati ya mawe makubwa.

**PAKA MWENYE MIGUU MIEUSI (BLACK – FOOTED CAT)**



Ni mdogo kuliko paka wa kufugwa. Hawa wanapatikana sana Afrika ya Kusini.
Huyu siye adui wa mkulima, kwa hali halisi ni kiumbe wa kupendeka.



Kwa asili anaonekana mwenye aibu siyo mkali. Anatembea pole pole na ni mwangalifu sana kwa nyendo zake lakini mwenye wasiwasi.

Nyayo za miguu ni mieusi kama lilivyo jina lake, unaweza kusema ni bahati ya pekee kumwona kwa macho kwa sababu ya tabia zake maalumu, mambo yake mengi hayafahamiki.

**LIGER NA TIGLON**



Tunakuja sehemu ya kuvutia kati ya paka mwenye manyoya ya shingoni kama simba na **tigress wa Bengal** anazalishwa na kupata tiger aliyekuwa anapatikana katika bustani za Bloenfontein hadi alipo kufa yapata mwaka 1980.

Huyu ni paka wa namna yake katika dunia. Hakuna aliyezaliwa kama huyu tangu hapo, tunaamini tu kuwa yawezekana siku za usoni paka mwingine wa ajabu ni Tiglon, ingawa siyo wa Afrika ya kusini tunahitaji tumtaje pia.

Zile bustani za kufuga wanyama kule Marekani alifugwa pamoja na samba ambaye alitokea Tilgon. Ingawa huyu chui na simba hawewezi kuishi pamoja,lakini katika nchi ya utumwa waliweza kuishi pamoja. Huu ni ukweli ambao hauwezi kurudiwa.

**WANYAMA WALIYOKO KUSINI MWA AFRIKA WANAOFANANA NA PAKA LAKINI SI PAKA**

Baadhi ya wanyama wanamajina ya paka, lakini si paka halisi mojawapo ni kwa mfano **“mangoose au meercat**” kicheche (polecale) kwa hali halisi hawa si paka. Hawana matendo kama ya paka, wala hawana asili ya paka ingawa wanataka kufanana na jamii ya paka.

**GENET**

1. Mnyama huyu anahusika pia na kundi la Genet anayetaka kufanana na paka, mwingine mdogo kama cheche, melesi, fungo nk.
2.







Genet Civet cat Meercat (musket jaatkat)

**PAKA WENGINE WA ULIMWENGU**

**TIGER – CHUI MKUBWA MWENYE MADOA YA MILIA**

**TIGER**



Wanapatikana India Asia. Anamadoa ya rangi ya njano na meusi, ni mnyama mwenye maficho ya udanganyifu lakini akijichanganya na mazingira yanayo mzunguka. Ni mnyama lakini wa mazingira ya kijani kibichi.

Tiger wa Bengal yeye ni mwembamba na mmoja kati ya wawili, aina ya Siberian ndiye mkubwa sana wanaishi katika milima ya baridi ya Siberia wao hawaangaishwi sana na hali ya ubaridi.

Chui huyu wa Bengali anarukia mawindo yake. Ni mnyama mwenye kunyatia, mara chache sana anaonekana na kusikika. Ni mnyama wa kutembea usiku zaidi na atashambulia anaogopa vitu vilivyosimama, akiwemo mtu, atamuua kama atapita njia yake.



Chui huyu apandi miti, meno yake yaliyo makali kama wembe yanapenya katika kifaru au tembo aliyejificha, kama atahitaji iwe hivyo anakula mnyama yeyote anayeweza kumkamata.
Ni mwongeleaji mzuri sana anaye patikana karibu na maji yanayoitwa matakatifu ya mto GANGES kule India.

Chui mkubwa wa Siberia ni kati ya paka wakubwa mwenye urefu wa futi 31/2 ana uzito wa zaidi ya kg 200. manyoya yake ni marefu na manene kumlinda na theluji inapondondoka. Ana macho ya ajabu ya kijani inayomfanya kuwa kiumbe wa ajabu sana.

Tofauti na Bengal harukii mawindo yake, bali ananyemelea na kumvamia kama alivyo chui duma. Anakamata na kunyonga shingo na kulivunja. Wale wazee wanajilinda wenyewe kwa kunasa mawindo kwa sababu kwao hili ni rahisi. Wengi wa hawa kwa vile wako pekee yao wanajulikana sana kwa kula watu.



Chui wa Bengal mkali



Chui wa Siberia mkubwa

**CHUI MWEUSI – BLACK PANTHER**



Huyu anajulikana kama chui mweusi au kondoo mweusi wa jamii ya paka ingawa kwa hali halisi ni paka mzuri ni wachache sana.

Katika ngozi yake nyeusi kuna alama kama za chui, unaweza kumkuta amechanganyikana na chui wengine. Wengine wana mwekwa katika daraja la chui halisi, wengine kama albino mwenye madoa doa.

Anaishi katika vichaka vinene, ni walaji sana wa wanadamu anapopata nafasi kati ya paka wote huyu ni mwalibifu au mwangamizaji sana.

**COUGAR**

Huyu ni paka wa Amerika ya kasikazini mara zingine anajulikana chafya, "**Duma" simba wa milimani. Ngurumo wa milimani paka anaye piga chui mwekundu, paka wa milima "mfalme wa paka" muuaji, simba wa Amerika, shetani wa milimani kwa bahati mbaya amekufa katika sehemu zingine za Amerika ya kusini.**



Ana mudu kuishi kwenye barafu akinyatia na mjanja wa kukwepa, mwanataaluma wa kukwea miti anaishi peke yake na mtembezi wa usiku zaidi. Ni vigumu sana kumwona. Anakula wanyama aina ya kongoni wanaopatikana zaidi Amerika wanaoishi kati yao. Ananyemelea kwa ujanja sana mawindo yake yaliyo karibu naye.

Kitu kizuri tu kwa aina ya paka huyu ni muuaji wa mbwa wabovu wa Amerika wanaojulikana. Anaua kila kitu kuanzia panya hadi ng'ombe anaua ili ale lakini harudii mizoga aliyouwa.



Anatoa mliyo mkali anapokutana na mwenzake wa jamii moja hata usiku. Anasauti kali kama mwanamke anayetaka kuuwawa, kitu pekee cha kukumbuka ni pale unapomsikika.

Angalia sana bunduki hiyo uliyo nayo toa nafasi kati yako na yeye, akihitaji kitu udhihikika na chakula, atashambulia zizi la mifugo na kuweka gharama zote juu ya kichwa chake.

Ni mnyama katili, mwenye ghadhabu na maisha yake yote ni ya jinsi hiyo. Mjeuri sana lakini hata mbwa aweza kumfukuza.

**JAGUA – CHUI DUMA**



Huyu ni paka wa Amerika ya kusini wakati mwingine anajulikana kama chui wa Amerika ya kusini. Anatembea wakati mwingine hadi kasikazini mwa Arizona New Mexico hata Amerika ya kati.

Huyu mnyama mzito amejengeka kweli na mzito lakini ana mwendo wa kasi kama mwanga. Ni moja ya paka wa kubwa sana wa Amrika.



Anapatikana karibu na maji mahali ambapo anajifurahisha kwa kuogelea ndani ya maji. Pia anajitayarishia chakula chake kutokana na mamba. Ana tabia ya kujificha kwenye vichaka na kusubiri kima ambao hawana taarifa naye na huwarukia kwa ajili ya chakula. Ngozi yake ni yenye rangiya madoa ya njano.



Ni mnyama pia anayependa kuishi peke yake wanapenda kuishi katika mianya ya miamba ya mawe ya mlimani, lakini nafasi inaporuhusu atashuka kutoka huko na kuja kula wanadamu kama hatapata chakula kingine. Ingawa wanamwonyesha katika mikanda lakini ni mara chache kumwona akiwa hai

**BOBCAT WA AMERIKA**



Huyu ni jamii halisi ya chui mwenye macho makali Lynx. Akiwa na masikio yenye vishungi, pia wakati mwingine anajulikana kama bay lynx

Wakati mwingine anaonekana kama paka aliyekua kupita kiasi, mwenye rangi ya kahawia nyekundu ananguruma (hisses) kufoka na kutema mate anapokuwa amekasirikia.

Jina hili amepewa kutokana na mienendo yake ya bobbing anayoifanya kama kitu kinachoungua kwa kuruka kumzunguka.

Ni mkali na mchokozi hatari sana ingawa wakati mwingine anaonekana kama panya wakubwa lakini yuko mbali kabisa kuonekana kama mmoja.

Ana miguu mirefu na minene anauwezo wa kutembea juu ya barafu kwa haraka.

**(LYNX) CHUI MWENYE MACHO MAKALI WA KANADA AU KASKAZINI**

Huyu ni mnyama aliyefunikwa na manyoya mengi yanayomlinda na baridi. Lakini koti lake hili limekuwa ndiyo anguko lake wakati anapowindwa bila huruma kwa ajili ya manyoya yake.

Sababu nyingi hapendwi sana na wanadamu kwa sababu anaua wanyama wao. Kimo chake ni sawa na mbwa wa alsation kwa kima akiwa na mkia wa bob akionyesha mgongo wake ukiwa umeinama kidogo na koti jepesi lenye weusi madoa madoa au mistari. Kulingana na kimo chake ni mwenye nguvu na ana uzito wa kilo 40 ana mbio za kasi sana anapowinda. Hawa wanapatikana kwa wingi Sweden, Norway kwa siku hizi.



Anatembea peke yake anaonekana mwenye aibu, mkweaji wa miti hodari, mwenye sharubu nyeusi nzito chini ya kidevu chake.

Ni swala la paka akimfukuza mbwa. Huyu paka lynx anapenda mbwa mwitu. Ni adui mkubwa wa mbwa mwitu wekundu.
Chakula chake kikuu ni panya, mbawala, sungura, ndege na wanyama wadogo. Anapokuwa ametengwa atararua mifugo.
Ni mnusaji mzuri wa harufu ya wanyama atamfuatilia umbali wa km nyingi.

Yupo paka mwingine anayeitwa paradel lynx – yeye ni mdogo lakini ni jamaa ya huyu. Ana mabaka baka ya kahawia nyekundu, hawaonekani sana wanajichimbia zaidi milimani na katika maeneo ya ulaya. Anaonekana zaidi anapotafuta chakula.



Jamii nyingine ya kundi hili la paka ni chui wa kiispania anafanana na wengine, inavyoonekana wako kadri ya jozi 150 kule Uhispania. Wanahitajiwa sana kuhifadhiwa



Jamii ya chui wa India – paka wa vichakani mwa India, Indian bush cat. Akiwa na vishungi kwenye masikio yake anaishi mahali ambapo paka hawapatikani mara nyingi karibu na maji anapopendelea. Ni mnene lakini madoa yake mazito sana



Lynx wa ulaya huyu ni jamii ya mwisho ya paka ni mkubwa, mwenye macho makali. Mkia mrefu na miguu mirefu, ni mnyama mwenye mabaka mabaka meusi akiwa na weupe chini ya tumbo lake. Anaishi msituni hajulikani vizuri.

European Lynx



**OCELOTE**

Wakati mwingine anaitwa (Tiger cut) huyu ni mnyama anayejulikana sana duniani, ana mabaka baka ya rangi ya njano na meusi yasiyo na mpangilio mzuri kwenye ngozi yake yanayompa mwonekano wa uzuri.



Wanaofugwa wanazaa vichanga vizuri, ni vyanzo vizuri na wajanja wana mbinu za kupata chakula anajifanya amekufa anapokuwa na kiu ya kima anayekuja kumchunguza wakati anakula anakimeza bila tatizo lolote.

Makao yake anayaweka alama na vitu vya ziada chakula chake ni wanyama, mbawala, swala, ndege wanaoishi karibu naye. Anawarukia hajui kukwea miti lakini anaruka kwenye barafu si hatari kwa binadamu.



Ni paka anayepatikana Amerika kusini tu wanaishi Jangwani.


**CHUI WA BARAFU (IRIBIS IN SOUTHERN SEBERIA)**



Huyu ni paka wa Asia ya kati na nchi ya Tibet. Anaishi katika vilele vya mlima, anapotembea anauburuza mkia wake kwenye nyayo ili asiache alama yoyote kwa yule anayemfuatilia, kando ya jina lake huyu si chui kamili.

Si hatari anaishi porini kwenye wanyama wachache mahali anakoweza kupata maeneo yake ya asili.
Ni mkubwa amefunikwa na manyoya yanayomfanya awe mkubwa kuliko anayoonekana anataka kufanana na Tiger kwa umbo lake na anavyotazama.

**PAKA MLA SAMAKI WA INDIA**
Paka mwingine wa kuvutia ni kutoka Bama India na China anaishi sehemu za maji maji au topetope, palipo konokono, nyoka na samaki.



Wakulima wanamfundisha kushika samaki atakao karibu na maji bila kujitikisa kimya akisubiri samaki; atapekeka mkono wake kwa kasi kama mwanga na kutoka na mawindo yake. Anakamata samaki wengi zaidi ya mahitaji yake. Ili hata bwana wake awe na ziada kwa mahitaji mengine.

**PAKA PORI WA ULAYA**



Anafikiriwa kuwa ni mkubwa zaidi ya yule paka wa kufugwa, hakika ni paka wa porini sawa na wa kwetu. Kwa hakika huyu si paka wa kufugwa, anapatikana karibu nchi zote za Ulaya. Lakini Uingereza na Scotland ni wengi zaidi wanaendelea sana kuadimika na kupungua kwa idadi. Yapaswa waifadhiwe vyema kabla ya kupotea. Ngozi yake ina weupe chini ya miguu yake na mabaka meusi juu ya mwili wake. Anamkia mnene, kichwa chake ni kikubwa na masikio mapana na fuvu bapa la mviringo na sharubu za kuvutia.

- Mwingine ni "awe – inspiring" mwenye kiu ya damu anakwaruza chini kwa woga na taswira za kushiriki na kwa kila mtu anaye msikia.
- Hashambulii mwanadamu hadi amchokoze, bali atamtishia.
- Anaishi kwa kula panya na vimnyama vidogo na kama hatawapata hawa ataingilia mifugo inayofugwa, ataua mmoja na kumburura kutoka eneo lile aliloulia.

Atarudi kila siku pale alipopata mawindo ni rahisi kumunasa.

Anaogelea vyema. Anahasira sana anathema, mate atanguruma nk. Wanajitemea na mara nyingi ni wa kujificha. Kama utamfuga ni rahisi kupendana na hawa wa kawaida na kuzaa machotara. Lakini mara nyingi ni kitu ambacho uwezekano wake ni mdogo.





Tunaye mwingine anayefanana naye anaitwa "paka pori wa Asia (Asia wild cat)" ni wa porini, wanafanana na wengine wanaopatikana pande za dunia. Anaonekana kama wa kufugwa kwenye picha, lakini uwe mwangalifu na hicho anachoona kuwa kama mpole. Anaundanganyifu sana, ni mwovu kama wenzake.

**PAKA MWINDAJI WA ULAYA**



Huyu paka kule Ulaya anaitwa mwindaji. Anaua ndege na nyoka kwa ajili tu ya kuua, lakini chakula chake ni panya, anaua ndege na nyoka na kuwaacha hapo.

Mambo yake mengi anayoyapendelea hayajulikani vizuri. Hapatikani Afrika.

**CHUI PAKA**
Huyu ni paka mzuri ambaye anasikia vizuri lakini haoni. Mwili wake unafanana na ule wa chui na ana macho makubwa ana mabaka meusi na mistari ya milia.

**BAADHI YA PICHA ZA PAKA AMBAO HAWAFAHAMIKI VIZURI DUNIANI**

Picha ya paka pori ambao tunawasikia lakini hawafahamiki vizuri

Small Tiger



Paka mwenye mkia mrefu wa BRAZIL



Paka wa Wagati wa Milima
Ya India



Paka wa Pampa Amerika ya kusini





Misty panther

Marble cat



**PAKA WA KUFUGWA**



Tuliongea sana juu ya paka wa porini. Hawa paka wa kufugwa wanajulikana sana kwetu kama (panther) wana afya wanapenda kupapaswapapaswa na wenzi wa kukumbuka mara kwa mara.

Paka hawa mara nyingi wanajulikana kama wasiyosikia, lakini hii inakuwa na mashaka kidogo unapowaita wanaitika milango yao ya kuonja na kugusa ni dhaifu sana lakini mlango wa kunusa ni mkali na wanaona vyema na kusikia. Paka hawa wamegawanyika makundi mawili, **wenye manyoya marefu na mafupi**

**PAKA MWENYE MANYOYA MAREFU (UAJEMI PERSIAN)**



Wenye rangi moja nzito

Persian au paka wa Angola, ni wazuri sana waliyo na manyoya marefu, wapo wa aina nyingi.

- Majina yao yanaendana na rangi zao, wamepambwa vyema
- Wana vichwa vikubwa na masikio mazuri madogo na macho ya mirabamiraba pua fupi, wafupi lakini wenye mkia mzito.

Wako pia makundi mawili wenye rangi moja nzito na waliyo na rangi mchangayiko.



Paka anayependwa sana Uajemi (Persian) na anayejulikana ni wa blue amevikwa ngozi ya kiblue. Macho yake kama ya dhahabu.

**Yuko wa rangi nyekundu**

Huyu ni kama mfalme wa Uajemi, nitheruji nyeupe siyo sufi mwenye koti nene. Ni vigumu kumfanya paka huyu kuwa msafi lakini bado wanafanya maajabu ya kupapasapapasa au kubembeleza ni wasumbufu.

Macho yao ni ya Blue si jambo la kawaida kuona jicho moja la paka ni blue mengine ni kijani

**WEUSI**

Ni kati ya paka wanaopendwa kufugwa

- Wenye imani za kishirikina wanadhani ni paka anayeleta baraka
- Ana macho ya shaba.

**Rangi ya maziwa**

Ni wazuri wana ngozi ya rangi ya maziwa, hivyo wanajoto sana

- Macho yao ni kama shaba
- Ni paka wasafi sana, wanajijali.

**Asiye wa kawaida – mwekundu**

Ana rangi ya uzurungi- mwekundu unaong'ara kwa vile rangi yake haipendezi sana, si maarufu




**Aina ya fedha**

- Ana ngozi inayong'ara kama fedha
- Hasa katika jua
- Anapendeza lakini hajulikani sana

**WALIYO NA RANGI MCHANGAYIKO**



Mwenye magamba kobe – ana rangi nyekundu, nyeusi na mchanganyiko wa rangi ya maziwa. Hafahamiki sana.

**MWENYE RANGI YA KAHAWIA**

Wana manyoya yanayotifautiana wana asili ya kupendwa hata leo.

**WENYE MISTARI MIEKUNDU**

Wa Ujerumani hawa wanaendelea kuwa mashuhuru, wamepata tuzo nyingi katika maonyesho.

Wenye mistari ya rangi ya fedha ya kikahawia

Wana uchangamfu wote kuwa paka anauwezo wa kutoa watu waliyo na paka wa aina hii mara nyingi hawabadilishwi kwa watu wengine.



Pia kuna wengine wenye gamba la kobe na weupe wa uajemi ambao ni tabaka la paka wa mbali. Tabaka lingine la paka ni wenye rangi ya moshi na wenye rangi ya aina ya maziwa.

**CHANTILLA**



Aina nyingine ya paka wazuri wa aina ya Uajemi (Persian) wamejitokeza hivi karibuni na huyu ni aina ya chantila mzuri.

Anaendelea kuchukua umashuhuri kwa ajili ya manyoya yake laini na marefu yanayopendeza.

Wana manyoya madogo madogo ambayo yanatumika kutengenezea kofia na makoti.

**PAKA MWENYE MANYOYA MAFUPI**



Hawa ni paka wa nyumbani pia wapo kwa aina nyingi ambao inakuwa vigumu kutambua wote. Tutaona wachache

**Russian** blue – mwenye manyoya mafupi

Hawa ni wakubwa kuliko wa Uajemi (Persian) wanaoonekana wakubwa kwa ajili ya manyoya waliyo nayo. Hawa wana masikio makubwa miguu mirefu na mkia.

**Paka weupe mwenye manyoya mafupi**

Mwenye rangi ya blue hawa ni wachache. Pia wapo wa rangi nyeusi kabisa.

Rangi ya blue ya kiingereza na kiasi na wenye rangi ya malaika

Huyu anakuwa wa aina tofauti anapatikana nchini kote, hawa wanapendwa sana, wazito na wenye macho ya kijani.



**P**

**paka wa rangi ya kahawia/udhurungi**

Hawa paka wa rangi ya kahawia wana mistari, wakati mwingine wana mistari mieusi inayopatana na kielelezo chake, wana macho ya kijani.

Hawa paka wa kahawia kawaida wana madoa ya rangi ya kijivu. Wakati huo wale wenye manyoya mafupi ya fedha wanavutia sana, lakini ni wachache wana koti la aina ya rangi ya fedha yenye weusi.

Yule mwenye mistari miekundu /kahawia mwenye tabaka alilo katika kichwa ikikimbusha juu ya mbwa wa pekires. Ni mwekundu mwenye kutengenezwa na rangi ya kahawia.

**MWENYE GAMBA LA KOBE**

Ni mweusi na rangi ya weupe wakati huo yule mweupe na ganda la kobe na macho ya shaba na vivuli vingi ambavyo ni vigumu kusonda rangi yake halisi.



**PAKA WA SIAMESE**



Mfalme wote wa paka atakuwa Siamese, paka wa kifalme kati ya paka wote wenye manyoya mafupi, ni mzuri mwenye asili ya kupendwa. Ana umbo la kati, ni paka wa aina yake mwenye miguu ya kujificha ya nyuma kuliko ile ya mbele inayompa mwendo wa aina yake. Ana manyoya ya aina yake mwenye mkia. Mlio wake ni wa aina yake. Anaweza kufundishwa maarifa mengi kama mbwa.

Ni mlinzi mwaminifu. Haruhusu mgeni kuingia ndani, macho yake ni ya blue na yana telemkia kwenye pua wako wazi wenye rangi ya udhurungi na miguu ya kikahawia, mkia na masikio. Uso wake unafunikwa na manyoya ya kikahawia yenye ulinzi hakika.

Paka huyu hapendi kuachwa peke yake siku zote anataka kuwa na wa kufuatana naye. Vitoto vya paka vinazaliwa vyeupe na rangi zingine zitatokea baada ya siku kadhaa.

**PAKA WA SIAMESE**

Wamepewa jina hilo kutokana na rangi yao, aina ya chocorate na madoa ya blue

Paka hawa wanakuwa mashuhuri sana kwa vile wanatabia ya kupenda, kando ya kuwa wa pekee. Wanahitaji uangalifu hasa wanapougua. Ni paka wazuri kwa watoto.



**Seal point siame**



**Chocolate point siame**

**PAKA WA BAMA NA UABESHI – ABYSSIAN – ETHIOPIA BURMESE NA ABYSUAN**

Kama Siamese tunapata paka aina ya burma toka nchi ya Buma na uabeshi, kule Ethiopia wameweza kuwekwa katika daraja kama paka wa Siamese wanchi hizo, ingawa hazihusiani na maeneo ya asili lakini wanapatikana duniani kote.




Paka wa Burma



Paka wa Ethiopia

Pia tunapata paka wa aina hii kule Hawaii wanaojulikana kama paka wa "Havara" , wakichuliwa toka visiwa hivyo na kutawanywa dunia nzima.




**Paka wa Harana**




**Caist husian**

**PAKA WA MANX**



Huyu ni paka wa mashariki ya mbali hana mkia, kwa asilia wanatoka katika kisiwa cha Man, lakini walisafairishwa katika mashua za biashara na paka wa maeneo hayo na kuzaliana na matokeo yake ndiyo paka wa aina hii.

Anaporuka anatembea kama panya, kwa njia hiyo akapata jina hilo. Wengi wanaamini kuwa walizaliana na panya ambayo ni vigumu kuipa haki ya kibiblia. Huyu paka wa “manx” ana tabaka mbili za manyoya mazito na tako la mvuringo kama chungwa. Hii linafanya kusiwe na aina ya mkia.



Ni paka 100% lakini ana mapungufu katika kuzaa, hivyo wapo katika rekodi ya tofauti kama hawatahifadhiwa watapotea. Hiyo itakuwa aibu kwa sababu si paka wa kawaida.

**PAKA WA MEXICO ASIYE NA MANYOYA**

Kati ya paka wa pekee yake ni paka wa Mexico hana manyoya. Kiujumla hana manyoya na ana mstari mdogo juu ya mgongo wake, lakini anafanana na paka wengine.



Ana rangi ya blue ya kijivu wakati  mwingine anaonekana kama hana manyoya. Huyu paka wa aina yake anatunzwa kama kipenzi, paka kule Mexico ya kati. Kutokana na ufahamu wetu huyu hajafika Afrika.

**MATUMIZI YA PAKA**

1. Kwa nini watu wanafuga paka?
2. Je wanafaida yoyote kando ya kuwa wanyama wakupendeza?



3. Wanasaidia kuondoa panya wanao kula nafaka zetu. Kama paka wasingekuwepo katika nchi zetu kungekuwa na hasara kubwa sana kwa mazao yetu.
4. Paka wanapendwa kwa vile pia wanaleta furaha na ushiriano kwa wazee, wagonjwa na watoto kwa vile wanapenda kukaa karibu na watu, pia ni sehemu ya vitu vya kawaida vya nyumbani. Sijui ulimwengu ungekuwaje kama wasingekuwepo paka wa kupendwa..
5. Katika ulimwengu wetu wa kisasa wa mavumbuzi na uchunguzi mbalimbali unoatendeka, paka wamekuwa sehemu kubwa ya Elimu, katika shule za udaktari wamefanya sehemu muhimu sana. Wanatumiwa sana kwa shughuli za elimu kufanya binadamu adumishe afya yake.
6. Paka pia wana upekee kwa kuletea wanadamu bahati, pia ni njia nyingine ya kumshukuru muumba wetu kwa kutupatia wanyama hawa wanaopendwa kuwa sehemu ya maisha yetu. Ni ishara ya pekee kwa pendo la Mungu kututunza pia kwa kutumia paka.
7. Paka wa porini wanaleta uwiano kati ya wanyama wa porini na wa kufugwa kwa kula baadhi ya wanyama.
8. Tokana dhambi uwiano huu unapaswa uwepo ni moja wapo ya uwezo wa Mungu. Muumbaji wetu anatambua wazi kuwa hii ni lazina kuwepo akaweka wanyama wala nyama.
9. Paka wa porini ni kivutio kikubwa cha utii wanapohifadhiwa katika mbuga zetu. Inaongeza pato la taifa. Na wale waliyofugwa katika mazingira madogo na watu binafsi ni pato kwao pia.
10. Watu wanakuja toka maeneo mbalimbali kuona vitu hivi vizuri, maumbile ya Mungu ambayo katika nchi yao havipo.

**NAMNA YA KUTUNZA VITOTO VYA PAKA**

Yapo mambo kadhaa unayopaswa kuyafahamu unapokuwa na paka nyumbani kwako
Kwanza:



Chagua ni aina gani ya kitoto cha paka unachopaswa kuwa nacho nyumbani kwako unayetaka kumtunza. Angalia gharama zote zinazohusisha kumtunza.

Paka wanategemea mwanadamu kwa yote katika matunzo. Ni muhimu kwamba wayapokee. Tuyatambue mahitaji yao na kuwatunza hadi wawe wakubwa.

Kwa asili paka ni wasafi siku zote wanafukia kinyesi chao wanapojisaida. Unapaswa uandae mahali pa mchanga watakapofukia uchafu wao wanapojisaidia.

- Paka wanahitaji chakula cha kutosha kila siku unahitajiwa kujua mahitaji ya aina ya paka uliyenaye leo viko vyakula vingi vinavyopatikana katika masoko lakini ni ya ghali.
- Paka anahitaji maji, wawekee maji mahali pake . Wanahitaji maziwa kama nyongeza, hakikisha vitu hivyo wanavipata.




- Paka anahitaji mazoezi ebu mruhusu mtoto wa paka kurukaruka, cheza naye wakati mwingine unaweza kutembea naye kama vuna uwezekano hakuna hatari yoyote.
- Mahali pao pa kulala panatakiwa kuwa safi.
- Watikise mahali wanapolala pasafishwe kila mara.
- Hakikisha kuwa wadudu wa kuwasumbua hawapo, viroboto na papasi, nyunyizia dawa.
- Wapatie chanjo na wakaguliwe mara kwa mara .
- Mpe utunzaji wa kutosha na uangalizi wa kutosha

**VISA VYA PAKA**
Unapaswa kutoa hadithi juu ya paka, hii halitakuwa gumu, tafuta vitabu vinavyohusu paka soma na elezea.
Toa uzoefu wako juu ya paka uliye naye.

**ANDROCLES NA SIMBA**
Katika hadithi za watumwa wa kirumi Androcles alikuwa anatembea katika mbuga, siku moja aliona kitu cha ajabu kwa mara ya kwanza hakujua namna ya kufanya au kutenda, aliona simba anarambaramba kiganja chake, anaunguruma lakini hakuwa ananijia mimi.

Akitambua namna mnyama huyu alivyomkali tena wa hatari bila kujua nini kilimfanya kuwa na maumivu makali hayo alipaswa kufikiri kwa haraka na kutenda kwa haraka.

Pole pole alimsogelea simba huyu katika maumivu yake bila kujua nini anategemea. Mtumwa huyu aliyekuwa anashangaa aligundua kuwa mnyama huyu hakumsogelea kwa namna yoyote.

Alimsogelea karibu na kugundua kuwa alikuwa amechomwa na mwiba mkubwa katika kiganja chake. Huyu simba aliyekonda hakuweza kuwinda. Alifupisha hali hiyo na akajisikia kuwa anapaswa kufanya kitu fulani kwa huyu mnyama ama sivyo atakufa kwa njaa.

Kwa ujasiri wote aliweza akavuta ule mwiba na kuuondoa. Simba yule alimramba safari nyingi kama anamshukuru na pole pole Androcles alimtendea kwa furaha na kumwondolea maumivu yake na alienda akiimba njiani. Kabla simba hajapotea machoni pake aligeuka nyuma akamwangalia simba aliyekuwa anaramba jeraha lake.

Miaka mingi baadaye kwa sababu kadhaa Androcles alitupwa katika pango la simba. Alipofika chini ya pango simba walimkimbilia, kila mmoja alimwangalia nini kitafuatia. Simba alisimama karibu na miguu yake, akamnusa akaanza kurambaramba mtumwa yule anianza kumusugua shingo lake kwa kutosheka kabisa. Simba akawa anainua kijanja chake na kuonyesha kovu.

Maadui zake hawakuelewa vyema jambo hili wakifikiri huyu mtu ni mzimu fulani toka mbinguni wakamwachia huru na kumuruhusu simba kurudi kwenye pango lake, siku zote huruma huzawadiwa.



**HITIMISHO**

Katika kukamilisha kila nishani utatambua kuwa muumbaji alikuwa na mpango wa kufanya uchaguzi kwa ajili yetu kuufurahia.

Hapo mwanzo wanyama walikuwa marafiki wao kwa wao na kwa wanadamu wote waliishi kwa furaha kama familia kubwa. Dhambi ilivuruga hali zote wakawa wakali na wakatili na kuwa maadui wao kwa wao na wanadamu.

Lakini wengine bado wamekuwa marafiki zetu. Yako mambo mengi tunayoweza kujifunza juu ya paka upendo wao, utii kwa wanadamu, utunzaji wao kwa watoto wao ni fundisho la pekee tunaloweza kulipata.

Bwana atakapokuja mara ya pili kutakuwa na urejeshwaji wa vitu vyote, kama ilivyokuwa mwanzo, ilivyokuwa imepangwa kuwa. Biblia inatuambia wazi simba na kondoo wataishi pamoja na wakiongozwa na mtoto mdogo.

Hebu tuwe waaminifu tuwe sehemu ya mbingu mpya na nchi mpya tukifurahia ahadi za Mungu. Tukiishi pamoja naye.

Hebu furahia Nishani hii.
Tembelea mbuga za wanyama – Mikumi, Serengeti, Tarangire nk. ulizia zaidi wanyama waliyoko Tanzania jifunze zaidi tabia zao.

Aliko Afisa nyama mkaribisheni awape habari za wanyama na tabia zao.Tembeleenli mbuga za wanyama

Furahia uumbaji wa Mungu

Kitabu cha viumbe ni cha pekee, chafunua uweza wa Mungu na ukuu wake.

Fundisha vijana kwa makini wajue ukuu wa Mungu.



Bwana akubariki.







